

Waitara: Acheni kupitisha mifugo katika barabara

Na Veronica Mheta,
Ngorongoro

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara amewataka wananchi wa vijiji ya Sale na Masusu vilivyo-wilayani Ngorongorona wingine kote nchini, kuacha araa moja kupitisha mifugo katiki ya barabara ili kuesha uharibitu wa tabaka la ni inayojengwa.

Amesema kupitisha mifugo katikati ya barabara wamo zinazojengwa kuhidisha nyuma shughuli za chumi sanjari na kuharibuka la lami linalomwagua. Waitara aliyesema hayo

katika ziara ya ukaguzi wa barabara eneo la vijiji vya la Sale na Masusu wilayani hapa inapojengwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami yenyerefu wa kilomita 420 na ikigharini Sh bilioni 87 kwa awamu ya kwanza inayejengwa kilomita 49.

Vipande vitatu vilivyo-baki vinasubiri mkandarasi atakayechaguliwa na serikali kwa ajili ya kuendelea na ujenzi hadi kufikia Mto wa Mbu. Barabara hiyo ya Mto wa Mbu hadi Loliondo eneo la Waso-Sale inajengwa kwa kiwango cha lami huku serikali ikiwa imetoo Sh bilioni 87.126 kwa ajili ya ujenzi huo.

Alisema ujenzi wa baraba-

ra hiyo unatoka eneo la Musoma, Nata, Sansate kupitia Mgumu hadi Mto wa Mbu utafungua fursa ya maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi na eneo la Ngorongoro.

Alisema endapo wananchi wataendelea kupitisha mifugo katika tabaka la lami, mifugo hao watabomoa na kuleta hasara.

Mkandarasi ambaye ni kampuni ya M/s China Wuyi Co. Ltd ameomba kuon-gezewa muda hadi Aprili mwakani ili kukamilisha kazi hiyo.

Naibu waziri huyo alisitisiza kazi zisizo za kitaalamu katika maeneo yanayopitiwa na mradi, wapewe kipaum-

bele wananchi wanaohitaji kuzifanya.

Alitoa rai kwa viongozi wa vijiji kuzungumza na wakandarasi wanaojenga miundombini mbalimbali ili wanaojenga kambi za muda, wazijenge kwa kiwango bora na imara ili wanapomaliza miradi ya kimkakati, majengo hayo yatumike kwa huduma za zahanati, vituo vya polisi na huduma nyngine za kijamii.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala, aliwataka wafugaji kuheshimu vibao vilivyo-wewa na Wakala ya Barabara Mkoa wa Arusha (Tanrods) na kuahidi kufuatilia suala

la ajira kwa wananchi walio katika maeneo jirani na ujenzi wa mradi wa barabara ya Sale hadi Waso ili kuondoa urasimu.

"Mradi huo ukikamilika utafungua fursa ya maendeleo kwa wananchi wa wilaya hii hivyo pia, naomba mzingatia sheria sambamba na kuacha tabia ya wizi wa mafuta maana Ngorongoro tunahitaji barabara ya lami na hiki ndicho kipaumbele chetu Wanangorongoro," alisema.

Meneja wa Tanroads Mkao wa Arusha, Reginald Massawe, alisitisiza kumsimamia vema mkandarasi huyo ambaye kwa sasa amefikisha asilimia 81 ya ujenzi wa

barabara hiyo kwa awamu ya kwanza.

Alitoa rai kwa Mangwala kuhakikisha wananchi wana-pewa elimu ya matumizi ya barabara ili kidhibiti vinyesi ya mifugo kuzaga juu ya barabara inayojengwa eneo hilo.

Mbunge wa Viti Maalum Mkao wa Arusha kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Zaitun Swai, aliiomba barabara hiyo ikamilike kwa wakati na kupunguza kero kwa wananchi wa wilaya hiyo hasa wanawake wakiwamo wajawazito wanaopata shida na kuhitaji huduma za ku-jifungua na nyngine zinazo-husu uzazi.

Habari Leo Uki. 17, Julai



ictoria mwaka
ni watu 200
isha. MV Spice
ia katika Bahau-
nzibar mwaka
yopatikana na
ra 243. Kivuko
zero kilizama
kuua watu

WHO inasema,
uhusiano
uzama majini
ia kwamba
a 90 ya vifo
iye nchi
Aprilis mwaka
Mataifa
dhia Julai 25
siku rasmi ya
hi zote duni-
atua stahiki
kanavyo na

a mwaka huu
azuilika, Chu-
nuku WHO
urugenzi
rgaret Chan
suala hili
mbuliwi ath-
maana ime-
ta ianzishwe
i kuongeza
ibiti ajali za



Ndaki ataka uadilifu ukusanyaji maduhuli

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa
Mifugo
na Uvuvi,
Mashimba Ndaki
amewataka watend-
aji wanaofanya kazi
ya ukusanyaji wa
maduhuli ya serikali
katika minada, mialo
na vituo vya ukaguzi
kuifanya kwa uamini-
fu na uadilifu.

Ameonya kuwa
serikali haiwezi kuen-
delea kuwa na mtend-
aji atayejihusisha na
vitendo vinavyosababi-
sha upotevu wa mapato
ya serikali.

Alisema hayo katika
Kikao cha Tathmini ya
Ukusanyaji wa Mad-
uhuli ya Serikali kwa
Mwaka uliopita na
kuweka malengo mapya
ya ukusanyaji mapato
kwa mwaka 2021/ 2022,
kilichofanyika jijini
Dodoma juzi.

Ndaki alisema ili
kufikia malengo ya
kukusanya Sh Bilioni
90 walizojiwekea kwa
mwaka huu wa fedha,
lazima wafanye kazi
hiyo kwa uaminifu na
uadilifu kinyume na
hapo, hawatafanikiwa.

"Katika kipindi
ambacho nimekuwa
hapa wizarani nimepata
taarifa nyangi kuhusu
baadhi yenu kujihusisha
na vitendo vya upotevu
wa mapato, acheni ku-
fanya hivyo kwa sababu
tukikugundua hatutawe-
za kuendelea na wewe,"
alisema.

Kwa mujibu wa wazi-
ri, kumekuwa na vitendo
vingi vya upotevu wa
maduhuli ya serikali vi-
navyofanywa na baadhi
ya maofisa wasiokuwa
waaminifu hali inayosa-
babisha serikali kutopata
mapato yanayostahili.